



Allegheny Health Network

LENGO

Lengo la sera hii ni kuwapa wagonjwa taarifa kuhusu Sera ya Msaada wa Kifedha ya Allegheny Health Network (AHN) ("Sera"). Sera hii inaeleza utaratibu wa kuamua kama mgonjwa anastahili kupata msaada wa kifedha kuhusiana na bili yake ya matibabu katika AHN, aina za msaada wa kifedha zinazopatikana kwa wagonjwa wanaokidhi vigezo, huduma zinazojumuishwa na zile zisizojumuishwa katika sera hii, pamoja na sera ya utozaji wa bili na ukusanyaji wa malipo inayohusu wagonjwa wanaostahili kupata msaada wa kifedha. Zaidi ya hayo, sera hii pia inaelezea baadhi ya vipengele vya utaratibu wa utozaji wa bili za wagonjwa na ukusanyaji wa malipo ambavyo ni muhimu kwa wagonjwa wanaoomba na kupata msaada chini ya sera hii.

WIGO WA SERA

Dhamira ya AHN inajumuisha kuwapa watu katika jamii uwezo wa kupata huduma za matibabu, ikiwa ni pamoja na wale ambao wanaweza kuwa na ugumu wa kulipia huduma kutokana na rasilimali ndogo za kifedha na mapato. AHN itatoa huduma za matibabu kwa hali za dharura bila ubaguzi, kwa watu wote bila kujali uwezo wao wa kulipia huduma hizo au ustahiki wao wa kupata msaada wa kifedha chini ya sera hii. AHN haitachukua hatua yoyote inayoweza kuwazuia au kuwakatisha tamaa watu kutafuta huduma za matibabu kwa hali za dharura. Sera hii inatumika kwa huduma zote za matibabu ya dharura na huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya zinazotolewa na hospitali za AHN, ikiwemo huduma zinazotolewa katika hospitali hizo na taasisi yoyote inayohusiana nazo kwa kiwango kikubwa (kama inavyofafanuliwa na Idara ya Mapato ya Ndani).

Hospitali za AHN zinazozingatia sera hii ni Allegheny General Hospital, Allegheny Valley Hospital, Canonsburg Hospital, Forbes Hospital, Grove City, Jefferson Hospital, Saint Vincent Hospital, West Penn Hospital, Wexford Hospital, AHN Harmar Neighborhood Hospital, AHN McCandless Neighborhood Hospital, AHN Brentwood Neighborhood Hospital, na AHN Hempfield Neighborhood Hospital. Tazama Kiambatisho C kwa orodha kamili ya watoa huduma ambao Sera hii inawahusu na ambao Sera hii haiwahusu.

Sera hii inafanyiwa mapitio ya mara kwa mara na inaweza kurekebishwa wakati wowote kulingana na mahitaji. Sera hii imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya AHN na Bodi ya Wakurugenzi ya hospitali husika ya AHN na Bodi hizo lazima zikubali mabadiliko yoyote muhimu kwenye Sera hii; hata hivyo, Bodi za AHN na hospitali za AHN zimempa idhini Afisa Mkuu wa Fedha wa AHN kufanya mabadiliko yoyote

kwenye Sera ambayo yanahitajika ili Sera iweze kuzingatia sheria husika na mabadiliko mengine yoyote yasiyo ya msingi anayoona kuwa ni ya lazima au yanayofaa.

UFAFANUZI

Kiasi Kinachotozwa Kwa Ujumla (AGB): AGB inafafanuliwa kama kiasi cha fedha ambacho kwa kawaida hutozwa kwa huduma za matibabu ya dharura au huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya kwa watu wenye bima inayolipia huduma hizo, kiasi hicho kikiwa kimeamuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 1.501(r)-5(b).

Kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani ya Marekani, AHN hutumia mbinu ya “Look-Back” (mbinu ya kuangalia taarifa za nyuma) ili kubaini AGB kwa huduma za matibabu ya dharura au huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya, kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho za Marekani (26 C.F.R.). Sehemu ya 1, 53, na 602. AGB huhesabiwa kwa kugawanya jumla ya kiasi cha madai yote ya AHN ya huduma za matibabu ya dharura na huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya ambayo yameidhinishwa na bima za afya za binafsi, Medicare malipo kwa kila huduma, na Medicaid katika kipindi cha miezi 12 iliyotangulia, kwa jumla ya gharama za jumla zinazohusiana na madai hayo. Rejelea Kiambatisho D kwa maelezo ya jinsi AGB ya hospitali inavyohesabiwa.

Kwa kuzingatia miongozo ya Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani ya Marekani, AHN huweka kikomo cha kiasi kinachotozwa kwa huduma za matibabu ya dharura au huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya zinazotolewa kwa watu wanaostahili kupata Msaada wa Kifedha. Baada ya kuthibitishwa kuwa wanastahili kupata Msaada wa Kifedha, watu hawa hawapaswi kutozwa kiasi kinachozidi AGB (kiasi ambacho kwa kawaida hutozwa kwa huduma hizo).

Umma unaweza kupata kwa urahisi taarifa kuhusu AGB na namna inavyohesabiwa, kwa maandishi na bila malipo, kwa kutembelea tovuti ifuatayo [<https://www.ahn.org/financial-assistance-ahn-bills>] au kwa kutuma ombi kwa njia ya maandishi kwa anwani ifuatayo:

Sera za Huduma ya Matibabu ya Hisani
Mkurugenzi wa Masuala ya Ushauri wa Kifedha
Allegheny Health Network
2 Allegheny Center, Suite 602
Pittsburgh, PA 15212

Baadhi ya Mali Zisizozingatiwa katika Tathmini ya Msaada wa Kifedha: Fedha za kustaafu zilizotengwa katika mifuko ya pensheni, akaunti za uwekezaji wa kustaafu, 401(k) au akaunti nyingine zinazofanana za

uwekezaji wa kustaafu, nyumba kuu ya makazi, pamoja na gari kuu linalotumika na familia, hazitajumuishwa katika hesabu za kubaini ustahiki wa kupata Msaada wa Kifedha.

Hali ya Dharura ya Kimatibabu: Imefafanuliwa katika Kifungu cha 1867 cha Sheria ya Hifadhi ya Jamii (42 U.S.C. 1395dd). Hali ya dharura ya kimatibabu hufafanuliwa kuwa hali ya kiafya inayojidhihirisha kupitia dalili za ghafla zenye ukali wa kutosha (ikiwemo maumivu makali, matatizo ya afya ya akili na/au dalili za matumizi mabaya ya vileo au dawa za kulevya), kiasi kwamba kutopata huduma ya matibabu mara moja kunaweza kutarajiwa kusababisha: (1) kuhatarisha kwa kiwango kikubwa afya ya mtu (au, kwa mwanamke mjamzito, afya ya mwanamke huyo au mtoto wake ambaye hajazaliwa); (2) kuathirika vibaya kwa utendaji wa mwili; au (3) kuharibika vibaya kwa utendaji wa kiungo chochote cha mwili au sehemu yake.

Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs): Zimefafanuliwa kuwa zinajumuisha yafuatayo kwa mujibu wa Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani ya Marekani:

- Kuuza deni kwa mtu au taasisi nyingine, isipokuwa katika hali fulani zilizoruhusiwa
- Kuripoti taarifa hasi kuhusu mkopo au historia ya malipo kwa mashirika ya kuripoti taarifa za mikopo au ofisi za taarifa za mikopo
- Kuchukua hatua zinazohitaji mchakato wa kisheria au wa kimahakama, ikiwa ni pamoja na, lakini bila kuzuiliwa na, yafuatayo:
 - Kuweka madai ya kisheria dhidi ya mali (isipokuwa katika hali fulani zilizoruhusiwa)
 - Kuchukua mali isiyohamishika iliyowekwa rehani kupitia taratibu za kisheria kutokana na kushindwa kulipa deni
 - Kuweka zuio au kukamata akaunti ya benki au mali nyingine yoyote ya kibinafsi
 - Kuanzisha shauri la madai mahakamani
 - Kusababisha mtu kukamatwa
 - Kumweka mtu chini ya amri ya mahakama ya kukamatwa na kuwekwa kizuizini
 - Makato ya mshahara

Familia: Kwa kutumia ufafanuzi wa Ofisi ya Sensa ya Marekani ni kundi la watu wawili au zaidi wanaoishi pamoja na ambao wana uhusiano wa kifamilia kwa kuzaliwa, ndoa au kuasiliwa kisheria. Kwa mujibu wa kanuni za Idara ya Mapato ya Ndani ya Marekani (IRS), ikiwa mgonjwa anamtaja mtu kama mtegemezi katika fomu yake ya kodi ya mapato, mtu huyo anaweza kuchukuliwa kuwa mtegemezi kwa madhumuni ya kupata Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii.

Mwongozo wa Serikali kuhusu Kiwango cha Umaskini: Mwongozo wa Serikali ya Marekani kuhusu Kiwango cha Umaskini ni mwongozo unaosasishwa kila mwaka katika Kumbukumbu Rasmi za Serikali (Federal Register) na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani, kwa mujibu wa mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha Kifungu cha 9902 cha Ibara ya 42 ya Kanuni za Marekani.

Msaada wa Kifedha: Kupunguzwa kwa gharama kikamilifu au kwa sehemu kwa huduma zinazotolewa kwa wagonjwa na hospitali za AHN, madaktari walioajiriwa na AHN, madaktari ambao hawajaajiriwa na

AHN, pamoja na mashirika mengine washirika yaliyoorodheshwa katika Kiambatisho C, kiasi cha punguzo kitaamuliwa kulingana na ustahiki wa mgonjwa chini ya mpango huu, ambao hutegemea vigezo vya ustahiki vilivyowekwa na AHN.

Mdhamini: Ni mtu mwingine tofauti na mgonjwa ambaye anawajibika kulipa bili au deni la mgonjwa iwapo mgonjwa atashindwa au hataweza kulipa bili au deni hilo.

Gharama za Jumla: Viwango rasmi vya bei vilivyowekwa na AHN na jumla ya gharama za kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa kabla ya kutumika kwa punguzo la gharama kutokana na mikataba (ikiwemo punguzo lililokubaliwa), makato mengine kutoka kwenye mapato, na malipo.

Mapato: Mapato ya familia yatajumuisha mishahara, malipo ya ukosefu wa ajira, malipo ya matunzo ya mtoto, majukumu ya kulipia huduma za matibabu, malipo ya matunzo kwa mtalaka, mapato ya hifadhi ya jamii, malipo ya mafao ya ulemavu, mapato ya pensheni au mafao mengine ya kustaafu, mapato ya kodi ya pango, mrabaha, mapato yatokanayo na mirathi na amana za uaminifu, fedha zinazotokana na hukumu za mahakama, gawio na mapato ya riba, pamoja na aina nyingine yoyote ya mapato yanayotozwa kodi, isipokuwa yale yaliyoondolewa waziwazi kama ilivyoelezwa katika hati hii. Baadhi ya vitu havitajumuishwa katika tathmini inayofanywa kwa mujibu wa Sera hii, ikiwa ni pamoja na thamani ya umiliki katika nyumba kuu ya makazi, akaunti za mipango ya kustaafu, amana za uaminifu zisizoweza kubatilishwa zilizowekwa kwa madhumuni ya mazishi, pamoja na mipango ya akiba ya elimu ya chuo inayosimamiwa na serikali ya kuu au serikali ya jimbo. Kwa wagonjwa walio chini ya umri wa miaka 18, mapato ya familia yanajumuisha yale ya wazazi na/au wazazi wa kambo, washirika ambao hawajaoa/kuolewa au washirika wa nyumbani (ambao wanaweza au wasiweze kuishi na mtoto mdogo).

Kwa madhumuni ya Sera hii, Mapato ya mwaka humaanisha makadirio ya mapato ya mtu kwa kipindi cha mwaka mmoja, yanayokokotolewa kwa kutumia taarifa za mapato zilizotolewa na mgonjwa. Kwa kawaida, Mapato ya Mwaka yataamuliwa kwa kupitia taarifa rasmi za hivi karibuni za kiasi hicho, kwa kukagua fomu za marejesho ya kodi, fomu za W-2, hati za malipo ya mishahara, na/au nyaraka nyingine zinazofaa za uthibitisho pamoja na taarifa zilizowasilishwa kwa AHN wakati wa mchakato wa maombi. Ikiwa itahitajika, AHN inaweza kutumia mbinu inayofaa ya kutathmini taarifa hizo za mapato ili kukadiria Mapato ya Mwaka pale ambapo taarifa za mapato za mwaka mzima wa hivi karibuni hazipatikani au ambapo mabadiliko ya hivi karibuni katika mapato ya mgonjwa yanahitaji kufanyiwa tathmini upya.

Hali za hivi karibuni, kama vile kupoteza kazi, kupata kazi mpya, kubadilisha kazi, n.k., zinaweza kuzingatiwa, pamoja na matumizi ya busara ya uamuzi wa AHN, kwa hiari ya AHN pekee, wakati wa kukokotoa Mapato ya Mwaka na kubaini ustahiki wa kupata Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii.

Mali au Fedha Taslimu: Mali au fedha taslimu zinajumuisha fedha taslimu, akaunti za kawaida, akaunti za akiba, akaunti za soko la fedha, amana za muda maalumu, mifuko ya uwekezaji wa pamoja, hati fungani na vyombo vingine vya kifedha vinavyofanana na hivyo vinavyomilikiwa na mgonjwa au mdhamini wa malipo. Mali au fedha taslimu zinazozidi kiasi kilichoonyeshwa katika Kiambatisho E lazima zitumike kulipia bili au deni lolote linalodaiwa na AHN kabla ya kustahiki kupata Msaada wa Kifedha.

Ugumu wa Matibabu: Kwa madhumuni ya Sera hii, mtu ambaye salio la gharama za matibabu analowajibika kulipa, baada ya kutumia mali au fedha zake zote taslimu na kuzingatia malipo ya bima pamoja na mafao mengine kutoka kwa wahusika wengine, linafikia au kuzidi asilimia 25 ya mapato yake ya mwaka, atachukuliwa kuwa amekumbwa na Ugumu wa Kifedha Unaotokana na Gharama za Matibabu.

Matibabu ya Lazima: Imefafanuliwa na Vituo vya Huduma za Medicare na Medicaid kuwa huduma au bidhaa zinazofaa na zinazohitajika kwa ajili ya kutambua au kutibu ugonjwa au jeraha.

VICEZO VYA KUSTAHILI KUPATA MSAADA WA KIFEDHA (NA UTARATIBU WA KUPOKEA)

1. Muhtasari wa Mchakato

Wagonjwa wanaoomba Msaada wa Kifedha watahitajika kupitia hatua kadhaa muhimu, ambazo kwa ujumla zimeainishwa hapa chini.

- A. Mgonjwa Anaelewa Vicezo vya Kustahili Kupata Msaada wa Kifedha na Kiwango cha Msaada Unaopatikana Chini ya Sera hii
- B. Mgonjwa Anakamilisha Mchakato wa Kutuma Maombi
- C. AHN Inakamilisha Tathmini ya Ustahiki wa Kupata Msaada wa Kifedha
- D. Ikiwa Maombi Yataidhinishwa, Msaada wa Kifedha Unawekwa kwenye Akaunti ya Mgonjwa

2. Vicezo vya Kustahili Kupata Msaada wa Kifedha na Aina za Msaada Unaopatikana

Makazi: Mgonjwa lazima awe raia wa Marekani au mkazi wa kudumu wa Marekani aliye na hadhi halali ya uhamiaji, na awe mkazi wa Jumuiya ya Madola ya Pennsylvania. Wagonjwa wa kimataifa wanaweza kustahili kupata Msaada wa Kifedha ikiwa wanakidhi vicezo vya kustahili kupata huduma za Medicaid. Kunaweza kuwa na hali maalum zinazowahusu wagonjwa kutoka nje ya jimbo na wagonjwa wa kimataifa (kwa mfano, ajali za magari au magonjwa yanayohitaji matibabu ya dharura), ambapo AHN, kwa hiari yake pekee, inaweza kuwazingatia wagonjwa hao kwa ajili ya kustahili kupata Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii.

Sharti la Mgonjwa Kutafuta Kwanza Vyanzo Vingine vya Ufadhili Vinavyopatikana: Ni lazima mgonjwa aonyeshe kuwa amejitahidi kwa nia njema kutuma maombi na kufuata taratibu za kupata huduma mbadala za afya zinazopatikana na zenye gharama nafuu (kwa mfano, sifa za kustahiki Medicaid na programu nyingine za ruzuku ya huduma za afya chini ya Sheria ya Huduma za Afya kwa Gharama Nafuu), au atoe ushahidi kwamba hatakidhi vicezo vya kustahiki kupata huduma kupitia Medicaid au programu nyinginezo.

- **Kukataa Kutafuta Vyanzo Vingine vya Ufadhili:** Msaada wa kifedha hautapatikana kwa wagonjwa wanaokataa kutumia chaguo za bima zinazopatikana kwao na kwa wagonjwa ambao hawajatumia kikamilifu vyanzo vyote vya malipo ya bima (kwa mfano, siku za akiba za maisha za Medicare).

Aina za Huduma Zinazogharimiwa Chini ya Msaada wa Kifedha: Msaada wa Kifedha utatumika tu kwa huduma za matibabu ya dharura na huduma nyingine za matibabu zinazohitajika kiafya. Baadhi ya huduma ambazo hazigharimiwi na Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii zimeainishwa katika Kiambatisho A. Msaada wa Kifedha hautapatikana kwa gharama zinazotokana na hali ambapo mgonjwa anakataa kuruhusiwa kutoka hospitalini na hivyo kusababisha gharama za ziada zinazochukuliwa kuwa si za lazima kiafya. Kuhusu gharama za dawa, punguzo la Msaada wa Kifedha linatumika tu kwa dawa zinazotolewa na AHN wakati wa kulazwa hospitalini au wakati wa kupata huduma kama mgonjwa wa nje. Punguzo hili halitumiki kwa dawa nyingine zozote au dawa zinazoagizwa kupitia huduma za kuagiza dawa kwa njia ya posta. Msaada wa Kifedha hautumiki kwa huduma ambazo zinapaswa kugharimiwa na kampuni ya bima lakini kampuni hiyo imekataa kulipia huduma hizo kutokana na mashauri ya kisheria, ukosefu wa ushirikiano toka kwa mgonjwa, au kupokea (au kutegemea) taarifa zisizo sahihi zilizotolewa na mgonjwa.

Vigezo vya Kiwango cha Chini cha Mahitaji ya Kifedha na Hesabu Yake: Kuna vigezo vikuu vitatu vya kifedha vinavyotumika kama ifuatavyo ili kubaini iwapo mgonjwa ana uwezo wa kifedha wa kulipa na iwapo anatimiza masharti ya kupata Msaada wa Kifedha kwa mujibu wa Sera hii, ikizingatiwa kuwa vigezo vingine vya Sera (kama vile makazi) pia vinatimizwa.

1. Kwanza, mali au fedha taslimu za mgonjwa hubainishwa (tazama ufafanuzi wa awali wa mali au fedha taslimu). Iwapo mali au fedha taslimu zinazidi kiwango cha kizingiti kilichokokotolewa na kuonyeshwa katika Kiambatisho E, basi mali zote zinazozidi kiwango hicho lazima zitumike kwanza kulipia salio lolote ambalo mgonjwa anadaiwa na AHN.
2. Hatua ya kwanza ikishakamilika, iwapo mgonjwa bado anadaiwa kiasi fulani cha fedha, basi atafanyiwa tathmini kulingana na kipato chake. Iwapo mapato ya familia ya mgonjwa na/au mdhamini yako katika kiwango cha 200% au chini ya hapo kulingana na Miongozo ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali (FPL), basi AHN itafuta 100% ya salio ambalo mgonjwa bado anawajibika kulilipa na ambalo linastahiki kupata Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii. Msaada wa Kifedha hautapatikana kwa mgonjwa au mdhamini wa malipo ambaye Mapato yake ya Mwaka yanazidi 200% ya FPL, isipokuwa kama anastahili kupata msaada chini ya kifungu cha Ugumu wa Kifedha Unaotokana na Gharama za Matibabu, kama ilivyoielezwa hapa chini. Rejelea Kiambatisho B kwa mwongozo wa sasa na jedwali la Kiwango cha FPL.
3. Kama mbadala wa hatua ya 2, mgonjwa anaweza kuthibitisha kuwa amekumbwa na Ugumu wa Kifedha Unaotokana na Gharama za Matibabu. Wagonjwa wanaokidhi vigezo vya Ugumu wa Kifedha Unaotokana na Gharama za Matibabu wanastahili kupata kiwango kilekile cha Msaada wa Kifedha kinachotolewa kwa watu ambao mapato yao yako chini ya 200% ya Miongozo ya FPL.

Kwa ujumla, AHN haitoi Msaada wa Kifedha kwa wagonjwa ambao mapato yao yanazidi 200% ya FPL, isipokuwa kama wanakidhi vigezo vya Ugumu wa Kifedha Unaotokana na Gharama za Matibabu.

AHN haitumii maamuzi yoyote ya awali kuhusu ustahiki wa kupata Msaada wa Kifedha kama msingi wa kuidhinisha moja kwa moja maombi ya Msaada wa Kifedha ya mgonjwa. Msaada wa Kifedha wa mgonjwa unapoisha, mgonjwa lazima atume maombi mapya ya kupata Msaada wa Kifedha. Kwa ujumla, baada ya kuthibitishwa kuwa anastahili, mtu ataendelea kustahili kupata Msaada wa Kifedha kwa kipindi cha miezi sita, baada ya hapo atahitajika kutathminiwa upya ili kuthibitisha ustahiki wake wa kupata Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii. Aidha, ombi la Msaada wa Kifedha lililowasilishwa na kuidhinishwa katika hospitali yoyote ya AHN litatumika katika hospitali zote za AHN, isipokuwa Hospitali ya Westfield Memorial.

3. Mchakato wa Maombi

Kwa ujumla, wagonjwa lazima wajaze fomu ya maombi ya Msaada wa Kifedha ya AHN ili maombi yao yaweze kuzingatiwa chini ya Sera hii.

Wagonjwa lazima wawasilishe hati moja au zaidi kati ya nyaraka zifuatazo za uthibitisho ili kuthibitisha mapato na/au mali zao:

- Fomu ya Kodi ya Mapato ya Serikali 1040 au fomu nyingine za serikali zinazotumika kuripoti kodi kwa mwaka uliopita (pamoja na maelezo kuhusu mabadiliko yoyote makubwa ya mapato)
- Nakala za hati za malipo (kwa siku 30 zilizopita)
- Uthibitisho wa maandishi wa mapato mengine yoyote yaliyopokelewa (kwa mfano, malipo ya talaka, matunzo ya mtoto, fidia ya ulemavu, pensheni, mapato ya kodi, uthibitisho wa mapato ya kujiajiri (taarifa ya faida na hasara kwa mwezi uliopita), hifadhi ya jamii, fidia ya ukosefu wa ajira, faida za VA, fidia ya mfanyakazi huweza kuombwa kama sehemu ya mchakato wa maombi)
- Taarifa za benki kutoka mwezi wa hivi karibuni kabla ya tarehe ya maombi ya Msaada wa Kifedha
- Notisi za kufilisika zinazofanya tarehe za kutolewa kwa huduma zihusishwe katika mchakato wa kufilisika
- Hati rasmi ya kiapo inayothibitisha taarifa za mapato na/au mali za mgonjwa au mdhamini wa malipo, zinazoonyesha kuwa anastahili kupata Msaada wa Kifedha
- Ikiwa inatumika na inapatikana, uthibitisho wa makazi katika makazi ya watu wasio na makazi au dalili ya kutokuwa na makazi

Maombi lazima yapokelewe ndani ya siku 240 kuanzia tarehe ambayo AHN ilituma kwa mara ya kwanza taarifa ya malipo baada ya kuruhusiwa kwa mgonjwa ("kipindi cha maombi"). Kushindwa kwa mgonjwa kuwasilisha maombi kamili au kushindwa kurejesha maombi ikijumuisha hati zote zinazohitajika za msaada ndani ya kipindi hicho cha maombi kunaweza kusababisha kukataliwa kwa Msaada wa Kifedha.

- Kipindi cha kutoa taarifa ni kipindi ambacho AHN inapaswa kumjulisha mtu kuhusu Sera hii. Kipindi hiki huanza katika tarehe ambayo huduma inatolewa kwa mtu binafsi na kuishia katika siku ya 120 baada ya AHN kumpa mtu binafsi taarifa ya kwanza ya malipo baada ya

kuruhusiwa kutoka hospitalini. Ikiwa mgonjwa atashindwa kuwasilisha maombi ya Msaada wa Kifedha kufikia mwisho wa kipindi cha kutoa taarifa, AHN inaweza kuchukua Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) kwa madhumuni ya kukusanya malipo ya deni lililo kwenye akaunti ya mgonjwa.

- AHN itapokea na kuchakata maombi yaliyowasilishwa na mtu binafsi katika kipindi kirefu cha maombi kinachoishia siku ya 240^{ya} baada ya AHN kumpatia mgonjwa taarifa ya kwanza ya malipo baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini.
- Maombi yoyote yanayohitaji maelezo ya ziada yatasababisha barua kutumwa kwa mgonjwa kuomba maelezo hayo ya ziada. Pia, simu inaweza kupigwa kwa mwombaji ili kumjulisha kuhusu maelezo ya ziada yanayohitajika. Ikiwa taarifa zote zinazohitajika kuthibitisha ustahiki wa mgonjwa hazitapokelewa ndani ya kipindi cha maombi cha siku 240, AHN inaweza kukataa ombi la Msaada wa Kifedha
- Maombi kamili ya Msaada wa Kifedha pamoja na nyaraka kamili zinazoambatana nayo yanapaswa kuwasilishwa kwa anwani ifuatayo. Idara ya Ushauri Masuala ya Kifedha inaweza kutoa taarifa kuhusu Sera hii na ina jukumu la kushirikiana na wagonjwa ili kubaini ustahiki wao wa kupata Msaada wa Kifedha

Uendeshaaji wa Mzunguko wa Mapato ya AHN
Ushauri wa Masuala ya Kifedha
2 Allegheny Center, Suite 602
Pittsburgh, Pa 15212

Wagonjwa wanaohitaji taarifa kuhusu Sera hii au msaada kuhusiana na ukamilishaji wa maombi wanapaswa kuwasiliana na Idara ya Ushauri wa masuala ya Kifedha AHN kwa nambari 1-855-493-2500.

4. Uamuzi wa Ustahiki wa Kupata Msaada wa Kifedha

Mara tu mgonjwa anapoidhinishwa, Msaada wa Kifedha hutolewa kwa kipindi cha miezi sita, kuanzia tarehe ya kuidhinishwa. AHN itatumia marekebisho ya Msaada wa Kifedha kwenye akaunti za awali ambazo ziko ndani ya kipindi cha siku 240 kuanzia tarehe ya taarifa ya kwanza ya bili iliyotumwa kwa mgonjwa baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini, ambayo ilisababisha kuwasilishwa kwa ombi la Msaada wa Kifedha. Hata hivyo, AHN inahifadhi haki ya kuweka mipaka ya utumiaji wa Msaada wa Kifedha kwa kipindi cha nyuma, kwa muda unaozidi kile kinachohitajika kwa ujumla chini ya Kifungu cha 501(r). Kwa ujumla, kizuizi hiki kitatumika tu pale ambapo kuna tofauti kubwa zisizo za kawaida kati ya hali ya kifedha ya sasa ya mgonjwa na hali yake ya kifedha katika kipindi cha miezi sita kabla ya kuidhinishwa kwa Msaada wa Kifedha, na ambapo tofauti hizo pia zinaambatana na ushahidi wa wazi kwamba fedha au mapato ya kutosha yalikuwepo katika kipindi hicho cha awali kulipia bili za matibabu ambazo hazijalipwa.

Punguzo la Msaada wa Kifedha linatumika tu kwa kiasi ambacho mgonjwa anawajibika kulipa; halitajumuisha kiasi chochote kinachodaiwa kutoka kwa kampuni za bima. Uamuzi wa kama mtu anastahiki Msaada wa Kifedha unaweza kujumuisha hali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na zifuatazo:

- Mgonjwa hana huduma ya Msaada wa Kimatibabu wala bima ya afya yenye kiwango cha kutosha cha kugharamia matibabu
- Mgonjwa ametumia kikamilifu faida zote za bima
- Bima ya msingi imetoa malipo lakini kuna dhima nyingine zinazopaswa kulipwa
- Mgonjwa anachukuliwa kuwa hana uwezo wa kifedha wa kulipia matibabu kutokana na ugumu wa kifedha unaosababishwa na gharama za matibabu
- Mali za mirathi zilizoachwa na mgonjwa aliyefariki zitatumika hadi (kuisha) kulingana na kiasi cha madeni yanayodaiwa
- Mgonjwa amewasilisha hukumu rasmi ya mahakama kuhusu kufilisika ambayo inaathiri wajibu wake wa kulipia huduma zilizotolewa katika tarehe husika
- Mgonjwa hana makazi au amethibitisha kuishi katika makazi ya watu wasio na makazi

AHN itashughulikia kwa haraka maombi yote ya Msaada wa Kifedha na kumtumia mgonjwa au mwombaji taarifa ya maandishi kuhusu uamuzi wake wa kustahiki kupata Msaada wa Kifedha ndani ya siku 14 tangu kupokea maombi **yaliyokamilika**.

AHN haitakataa ombi kwa msingi wa mwombaji kushindwa kutoa taarifa au nyaraka, isipokuwa taarifa au nyaraka zilizoainishwa katika Sera hii au katika fomu ya maombi ya Msaada wa Kifedha.

Mgonjwa anaweza kuomba uamuzi wowote wa AHN wa kukataa kutoa Msaada wa Kifedha upitiwe upya. Mgonjwa lazima awasilishe ombi la kupitia upya uamuzi huo, kwa njia ya mdomo au kwa maandishi, ndani ya siku 30 tangu kupokea taarifa ya kukataliwa kwa Msaada wa Kifedha. Mara tu AHN inapokea ombi la mapitio, mapitio hayo yatafanywa na mwanachama wa uongozi wa Idara ya Ushauri wa Masuala ya Kifedha au mtu aliyeteuliwa naye ndani ya siku 30, kulingana na kupokelewa na kuhakikiwa kwa taarifa yoyote ya ziada inayohitajika ili kukamilisha mapitio hayo ya kufikiriwa upya yaliyoombwa.

Ikiwa idhini ya Msaada wa Kifedha itasababisha kuwepo kwa salio la ziada la fedha katika akaunti ya mgonjwa (yaani, salio la ziada linalotokana moja kwa moja na malipo ya awali yaliyofanywa na mgonjwa au kwa niaba yake kwa ajili ya sehemu ya bili ambayo mgonjwa anawajibika kulipa), basi mgonjwa au mpokeaji husika wa malipo (kulingana na hali ilivyo) atarejeshewa malipo yote husika yaliyofanywa na mgonjwa kwa huduma za matibabu zilizotolewa katika kipindi ambacho Msaada wa Kifedha umeidhinishwa. Hata hivyo, marejesho hayo yatafanyika tu kwa akaunti au tarehe za kutolewa kwa huduma ambazo Msaada wa Kifedha unatumika mahususi.

Marekebisho yoyote ya akaunti ya mgonjwa yanayotokana na kuidhinishwa kwa Msaada wa Kifedha lazima yaidhinishwe na wafanyakazi husika wenye mamlaka katika AHN. Marekebisho ya akaunti ya mgonjwa (kulingana na gharama za jumla) yaliyopendekezwa chini ya Sera hii lazima yawe na viwango vifuatavyo vya idhini:

Mwakilishi Aliyeteuliwa wa Idara ya Ushauri wa Masuala ya Kifedha	\$0-\$10,000
Mkurugenzi wa Ushauri Masuala ya Kifedha	\$10,001 hadi \$50,000
Makamu wa Rais Mzunguko wa Mapato	\$50,001 hadi \$100,000

Afisa Mkuu wa Fedha wa AHN au mwakilishi wake aliyeteuliwa atapitia na kuidhinisha marekebisho yote ya akaunti za wagonjwa yanayozidi \$250,000 yanayohusiana na Msaada wa Kifedha.

5. Uamuzi wa Ustahiki kwa Msingi wa Tathmini ya Awali

AHN inaelewa kuwa baadhi ya wagonjwa wanaweza kushindwa kukamilisha ombi la Msaada wa Kifedha, kutimiza maombi ya kuwasilisha nyaraka, au kwa namna nyingine kutoshiriki katika mchakato wa maombi. Matokeo yake, kunaweza kuwa na hali ambazo mgonjwa anathibitishwa kustahiki Msaada wa Kifedha bila kukamilisha maombi rasmi ya Msaada wa Kifedha. Katika hali hizi, hospitali za AHN zinaweza kutumia vyanzo vingine vya habari kufanya tathmini ya mtu binafsi ya mahitaji ya kifedha. Taarifa hii inaweza kuiwezesha AHN kufanya uamuzi sahihi kuhusu mahitaji ya kifedha ya wagonjwa wasiojibu mawasiliano, kwa kutumia makadirio bora zaidi yaliyopo pale ambapo hakuna taarifa zilizotolewa moja kwa moja na mgonjwa.

AHN inaweza kutumia wahusika wengine kufanya mapitio ya taarifa za mgonjwa ili kutathmini mahitaji ya kifedha. Mapitio haya hutumia mfumo unaotambuliwa katika sekta ya huduma za afya, ambao unategemea hifadhidata za kumbukumbu za umma. Mfumo huu wa uchambuzi hutumia data kutoka kwenye kumbukumbu za umma ili kukokotoa alama ya uwezo wa kijamii, kiuchumi na kifedha, inayojumuisha makadirio ya mapato, mali na uwezo wa kupata fedha taslimu kwa urahisi. Teknolojia hii imeundwa kutathmini kila mgonjwa kwa kutumia viwango ambavyo kwa ujumla tunatumia chini ya Sera hii na hutumiwa wakati taarifa mahususi haipatikani kutoka kwa mgonjwa.

AHN itachukua hatua za kupitia mara kwa mara mchakato huu wa kubaini ustahiki kwa makadirio na kutathmini ikiwa mchakato huo unasababisha maamuzi kuhusu maombi ya Msaada wa Kifedha ambayo yanakubalika na AHN, pale ambapo mgonjwa hawezi kukamilisha utaratibu wa kawaida wa kuwasilisha maombi.

Teknolojia hiyo ya wahusika wengine inapotumika kama msingi wa kubaini ustahiki kwa makadirio, punguzo linalotolewa chini ya Sera hii litatolewa kwa huduma zinazostahili kwa tarehe mahususi ya kutolewa kwa huduma pekee na mgonjwa atajulishwa kuhusu uamuzi huo na manufaa anayostahili kupata katika hali ambazo utoaji wa taarifa hiyo unahitajika kwa mujibu wa kanuni husika.

6. Baadhi ya Masuala ya Utozaji wa Bili na Ukusanyaji wa Madeni Yanayohusiana na Msaada wa Kifedha

AHN inajitahidi kupata malipo yote stahiki kutoka kwa wahusika wengine kwa ajili ya huduma zilizotolewa, ili kupunguza mzigo wa kifedha kwa mgonjwa na AHN. Wakati bima au ugharamiaji kutoka kwa wahusika wengine unashindwa kugharamia huduma zilizotolewa, au wakati hakuna bima au ugharamiaji wa wahusika wengine unaotumika, AHN inatarajia mgonjwa kulipa kiasi kinachostahili kwa huduma alizopewa, isipokuwa kama mgonjwa anapokea Msaada wa Kifedha chini ya Sera hii. Sera za AHN kuhusu utozaji wa bili na ukusanyaji wa madeni zitazingatia kanuni na sheria za serikali na majimbo zinazosimamia utozaji wa bili na ukusanyaji wa madeni katika sekta ya huduma za afya.

AHN inaweza kuchukua hatua za kawaida za ukusanyaji wa madeni (pamoja na Hatua za Kipekee za Kudai Malipo ECAs) dhidi ya wagonjwa waliobainika kutostahili kupata Msaada wa Kifedha, au wagonjwa ambao wameacha kushirikiana kwa nia njema katika kulipa kiasi cha fedha wanachodaiwa.

Kwa kawaida, AHN hutumia utaratibu wa kawaida wa ukusanyaji wa malipo kwa sehemu ya salio la akaunti ambayo mgonjwa anawajibika kulipa. Ikiwa sehemu ya salio la akaunti ambayo mgonjwa anawajibika kulipa itabaki bila kulipwa baada ya juhudi za kawaida za ukusanyaji wa malipo, Ofisi ya Usimamizi wa Mzunguko wa Mapato ya AHN itapanga au kupendekeza salio hilo ambalo halijalipwa liainishwe kama deni lisiloweza kukusanywa (bad debt), kwa mujibu wa sera na taratibu zake zilizowekwa.

Baada ya akaunti kuainishwa kuwa deni lisiloweza kukusanywa (bad debt), AHN inaweza kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea na mchakato wa ukusanyaji wa deni hilo. AHN inaweza kutumia ECAs ili kukusanya deni kwenye akaunti hiyo. Hata hivyo, AHN, kwa hiari yake pekee, inaweza kuchagua kutumia mbinu za kustahiki zinazodhaniwa kuwa za lazima ili kubaini ustahiki wa Msaada wa Kifedha kabla ya kufuata ECA zozote zinazohusiana na akaunti ambapo hakuna maombi ya Msaada wa Kifedha yaliyofanywa na mgonjwa. Ikiwa mgonjwa atakidhi vigezo vya kustahili kupata Msaada wa Kifedha kwa kutumia tathmini ya awali, basi hakuna Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) zitakazoanzishwa, na juhudi za kukusanya deni kwenye akaunti hiyo zitasitishwa.

Akaunti za wagonjwa walioidhinishwa kustahili kupata msaada hatimaye zitaainishwa kama huduma za matibabu zinazotolewa kwa hisani chini ya Sera hii. Akaunti hizo hazitapelekwa kwa mashirika ya ukusanyaji wa madeni, hazitachukuliwa hatua nyingine za kukusanya madeni, na hazitajumuishwa katika gharama za hospitali zinazotokana na madeni yasiyoweza kukusanywa.

Sera ya AHN kuhusu utoaji wa huduma kwa hali za dharura za kiafya inakataza kudai malipo kabla ya huduma kutolewa, au shughuli za kudai malipo zinazoweza kuingilia kati utoaji wa huduma ya dharura ya kiafya.

Hakuna ECA itakayofuatiliwa dhidi ya mgonjwa yeyote ndani ya siku 120 tangu kutumwa kwa taarifa ya kwanza ya malipo baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini na bila kwanza kufanya juhudi zinazofaa kubaini ikiwa mgonjwa huyo anastahiki Msaada wa Kifedha. Idara ya Ushauri Masuala ya Kifedha ya AHN ina jukumu la kubaini ikiwa juhudi zinazofaa zimefanyika ili kuthibitisha kama mgonjwa anastahili kupata Msaada wa Kifedha kabla ya kuanzisha Hatua zozote za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs). Juhudi zinazofaa zitajumuisha, lakini hazitazuiliwa kwa:

- Kuthibitisha kwamba mgonjwa anawajibika kulipa bili ambazo hazijalipwa, na kwamba vyanzo vyote vya malipo kutoka kwa wahusika wengine vimetambuliwa na AHN na bili husika zimewasilishwa kwa wahusika hao
- Kuweka marufuku dhidi ya hatua za kudai malipo kwa mgonjwa asiye na bima, hadi hapo mgonjwa atakapofahamishwa kuhusu Sera hii na kupewa fursa ya kuomba Msaada wa Kifedha
- Kumjulisha mgonjwa kwa maandishi kuhusu taarifa au nyaraka zozote za ziada zinazopaswa kuwasilishwa ili kubaini uhalali wa kupata Msaada wa Kifedha

- Kuthibitisha iwapo mgonjwa aliwasilisha maombi ya bima ya afya kupitia Medicaid au programu nyingine za huduma za afya zinazofadhiliwa na umma, na kupata nyaraka zinazothibitisha uwasilishaji huo
- AHN haitachukua Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) wakati ombi hili la kupata bima ya huduma za afya bado linasubiri uamuzi, hata hivyo, mara tu uamuzi kuhusu bima hiyo utakapofanywa, hatua za kawaida za ukusanyaji wa madeni zitaendelea, mradi tu mgonjwa hastahili kupata manufaa mengine yoyote chini ya Sera hii
- Kumtumia mgonjwa taarifa kwa njia ya maandishi kuhusu Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) ambazo AHN inaweza kuanzisha au kuendelea kuzitekeleza ikiwa mgonjwa hatakamilisha maombi ya Msaada wa Kifedha
- Kumtumia mgonjwa taarifa kwa njia ya maandishi kuhusu Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) ambazo AHN inaweza kuanzisha au kuendelea kuzitekeleza ikiwa malipo yanayodaiwa hayatapokelewa ndani ya siku 30 tangu tarehe ya kutumwa kwa taarifa hiyo kwa njia ya maandishi

Kwa mujibu wa miongozo ya serikali, AHN inaruhusiwa kuchukua Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) baada ya kipindi cha siku 120 cha kutoa taarifa, kuanzia tarehe ambayo taarifa ya kwanza ya bili baada ya mgonjwa kuruhusiwa kutoka hospitalini ilitumwa kwa mgonjwa. Hata hivyo, wakati wowote ndani ya kipindi cha siku 120 baada ya kumalizika kwa kipindi cha awali cha siku 120 cha kutoa taarifa, AHN itapokea na kushughulikia ombi la Msaada wa Kifedha kutoka kwa mgonjwa. Katika kipindi hicho, juhudi za kuchukua Hatua za Kipekee za Kudai Malipo (ECAs) zitasitishwa hadi uamuzi utakapofanywa kuhusu iwapo mgonjwa anastahili kupata Msaada wa Kifedha. Kwa hivyo, jumla ya kipindi ambacho AHN itapokea na kuchakata maombi ya Msaada wa Kifedha ni siku 240 kuanzia tarehe ya taarifa ya kwanza ya malipo baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini iliyotumwa kwa mgonjwa.

Hakuna wakala wa ukusanyaji wa madeni, kampuni ya uwakili, au mtu binafsi anayeruhusiwa kuanzisha hatua za kisheria dhidi ya mgonjwa kwa kutolipa bili ya AHN bila kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Afisa Mkuu wa Mzunguko wa Mapato wa AHN au mwakilishi wake aliyeteuliwa.

Katika tukio la kufilisika kwa mgonjwa, mara tu AHN inapopokea ushahidi wa kufilisika, hatua za ukusanyaji zitakoma mara moja kwa salio lililolipwa kwa huduma zote zilizotolewa kabla na hadi tarehe ya kufilisika.

KURIPOTI MSAADA WA KIFEDHA

AHN itazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za serikali, jimbo, na serikali za mitaa pamoja na mahitaji ya kuripoti yanayohitajika kwa shughuli zinazofanywa kwa mujibu wa Sera hii.

Michakato na taratibu za Msaada wa Kifedha zitapitiwa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa Sera hii inatekelezwa kama ilivyoielezwa humu.

Usimamizi wa Idara ya Ushauri Masula ya Kifedha ndiyo idara kuu ya ndani inayowajibika kwa ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa zinazohusiana na Msaada wa Kifedha, chini ya usimamizi wa Afisa Mkuu wa Mzunguko wa Mapato na kwa kushirikiana na mdhibiti wa fedha wa AHN.

UCHAPISHAJI WA SERA

Sera hii itapatikana katika lugha kuu zinazozungumzwa katika maeneo ya huduma ya kila hospitali ya AHN inayohusika na Sera hii. Nakala za karatasi za Sera hii, fomu ya maombi, na muhtasari wa Sera hii ulioandikwa kwa lugha rahisi zitapatikana bila malipo kwa yeyote atakayeziomba katika maeneo maalum ya umma ndani ya majengo ya hospitali, ikiwemo angalau katika chumba cha dharura (kama kipo) na maeneo ya usajili na upokeaji wa wagonjwa pamoja na kutumwa kwa njia ya posta. AHN itatumia mabango ya kawaida na vipeperushi kuwafahamisha wagonjwa na wageni kuhusu upatikanaji wa nyaraka hizi, kwa njia inayotarajiwa kuwafikia wanajamii ambao wana uwezekano mkubwa wa kuhitaji Msaada wa Kifedha. Aidha, Sera hii, pamoja na fomu ya maombi na muhtasari wake ulioandikwa kwa lugha rahisi kueleweka, vinapatikana kwenye tovuti ya AHN (<https://www.ahn.org/financial-assistance-ahn-bills>).

MAREJELEO

Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani

Kanuni ya 26 ya Serikali 1.501(r)-1 hadi 1.501(r)-7

Sera ya AHN ya Matibabu ya Dharura na Sheria ya Kazi (Kitambulisho cha sera 2538428).

VIAMBATANISHI

Kiambatisho A: Huduma Zisizojumuishwa katika Sera ya Msaada wa Kifedha

Kiambatisho B: Miongozo ya Serikali ya Umaskini

Kiambatisho C: Orodha ya Watoa Huduma Wanaotoa Huduma za Dharura au Huduma Nyingine za Kimatibabu Zinazohitajika

Kiambatisho D: Hesabu ya AGB ya Kituo cha Allegheny Health Network

Kiambatisho E: Kiasi cha Mali au Fedha taslimu

Saini/ Tarehe
Afisa Mkuu wa Fedha

Saini/ Tarehe
Afisa Mkuu wa Mzunguko wa Mapato